

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBAWANGA

SHULE YA SEKONDARI KILIMANI MAWENI,
S.L.P 671,
SUMBAWANGA.
TAREHE.....

Kumb. Na KMSS/12/2021/VOL.07

JINA LA MWANAFUNZI.....

S.L.P

SUMBAWANGA.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KILIMANI MAWENI KWA
MWAKA WA MASOMO 2021.

1. Utangulizi

Ninayo furaha kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha Kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya Sekondari Kilimani Maweni ipo umbali wa kilometa sita (06) toka Makao Makuu ya Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga. Muhula wa kwanza wa masomo utanza tarehe **11/01/2021**. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2021** (ndani ya siku saba).

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 Sare za Shule

(a) Wavulana

- i. Suruali mbili rangi ya **Karoti** zenye mkunjo chini size 17
- ii. Mashati mawili meupe tetroni mikono mifupi
- iii. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba na vyenye visigino vifupi
- iv. Sweta la Damu ya Mzee lenye ukosi wa V.
- v. Soksi nyeupe jozi mbili

(b) Wasichana

- i. Sketi mbili rangi ya **Karoti** yenye malinda sita ndefu (mazingira yetu yana upepo mkali)
- ii. Mashati mawili meupe tetroni mikono mifupi
- iii. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba vyenye kisigino kifupi
- iv. Soksi nyeupe jozi mbili
- v. Sweta la Damu ya Mzee lenye ukosi wa V.

(c) Kwa Waislam

Rangi ya hijabu ifanane na rangi ya sketi.

(d) Sare ya michezo kwa shule hii ni:-

Wavulana:

- i. Raba jozi moja
- ii. Truck suit na Bukta nyeusi zenye mistari

Wasichana:

- i. Raba jozi moja
- ii. Truck suit nyeusi zenye mistari

Vitu vingine vya kuja navyo:

2.2 Daftari kubwa (**Counter book quire two**) kumi na moja (11), kalamu na mkebe wa hesabu,

2.3 Vifaa vya usafi kama ndoo ndogo, Fagio na Jembe.

3.0 Sheria na kanuni muhimu za shule hii:-

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana na Elimu nchini chini ya **Ofisi ya Rais (TAMISEMI)**. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

- (a) Heshima kwa viongozi, walimu, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- (c) Kushiriki kwa makini katika kufanya maandalio ya jioni (preparations)
- (d) Kuwahi katika kila shughuli na nyinginezo utakazopewa
- (e) Kuwepo ndani ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- (f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- (g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
- (h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
- (i) Kutunza mali za umma.

3.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule:

- (a) Wizi
- (b) Uasherati na ushoga
- (c) Ubakaji
- (d) Ulevi na Matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
- (e) Kupigana au kupiga
- (f) Kudharau bendera ya Taifa
- (g) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- (h) Kuwa mjamzito / kupata mimba
- (i) kuo au kuolewa
- (j) Kutoa mimba
- (k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- (l) Kukataa adhabu kwa makusudi
- (m) Kuwa na simu ya mkononi

4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi ni:-

- (a) **Medical Examination Form** (Fomu ya uchunguzi wa Afya ya Mwanafunzi) ambayo itatajizwa na Daktari katika ofisi ya Manispaa ya Sumbawanga. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
- (b) **Fomu ya Maelezo binafsi** kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- (c) **Fomu ya mzazi kukiri** kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
- (d) **Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

KARIBU SANA KILIMANI MAWENI SEKONDARI

.....
PUDENSIANA J. KAMBOLE
MKUU WA SHULE

HISTORIA YA MWANAFUNZI

Jina la mwanafunzi

Jina la baba

Jina la mama

Shule ya msingi aliyosoma

Kijiji atokacho kitongoji cha

Tarehe ya kuzaliwa DiniDhehebu

Kabila

UTHIBITISHO:

5.1 Ahadi ya Mwanafunzi

Mimi nakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na kidato cha mwaka Katika shule ya Sekondari Kilimani Maweni, na ninaahidi:-

- i. Kuzingatia taratibu na kanuni zote za shule
- ii. Kuweka bidii katika masomo yote
- iii. Kushiriki katika shughuli za elimu ya kujitegemea
- iv. Kuwa na nidhamu ya juu ndani na nje ya shule

Jina

Sahihi

Tarehe

5.2 Ahadi ya Mzazi / Mlezi

Mimi mzazi / mlezi wa

Naahidi kwamba:

- i. Nitatimiza gharama za mwanangu kama nilivyoelekezwa
- ii. Nitamhimiza mwanangu kuzingatia taratibu za shule pamoja na masomo
- iii. Nakubaliana na kanuni na sheria zilizotolewa na serikali juu ya mwanafunzi (mwanangu)

Jina

Sahihi

Tarehe